

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

10/10/2018

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA KUWAKAANGA WATENDAJI MABASI YA MWENDOKASI KESHO, NI KUFUATIA USAFIRI HUO KUGUBIKWA NA KASORO ZINAZOWAUMIZA WANANCHI.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda amewaagiza watendaji wote wanaosimamia Usafiri wa Mabasi ya Mwendo wa haraka UDART kukutana nae kesho Alhamis Saa 12:30 Asubuhi eneo la kituo cha Mabasi (Kimara Bus Terminal) ili wamueleze kwanini hakuna hatua madhubuti walizochukuwa kumaliza kero za wananchi.

RC Makonda amesema kuwa hafurahishwi hata kidogo na namna mradi wa mabasi ya mwendo wa haraka unavyoendeshwa kwakuwa hata matarajio ya Rais Dkt. John Magufuli yalikuwa ni kuona changamoto ya muda mrefu ya usafiri inageuzwa kuwa historia kupitia mradi huo lakini imekuwa tofauti na matarajio hayo.

"Sifurahishwi na namna mradi wa Mwendokasi unavyoendeshwa kwani hata matarajio ya Mh. Rais Magufuli yalikuwa ni kuona changamoto ya muda mrefu ya usafiri kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam ikigeuzwa historia kupitia mradi huu, sasa hatuwezi kuvumilia kuona wananchi wanateseka wakati serikali yao ipo kwaajili yao, kesho lazima hili liishe ili wananchi wasafiri pasipo udumbufu Kama serikali yao inavyotaka".
Alisema RC Makonda.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM